MWONGOZO WA USAHIHISHAJI - SOMO LA KISWAHILI

KIDATO CHA TATU 2021

01

i	ii	iii	iv	v	vi	vii
a	b	e	d	a	b	c

Alama 7 @ 1

02 Mtahiniwa afupishe habari aliyoisoma kwa kuzingatia

i/ Kichwa cha habari alama 02
ii/ Lengo/kiini cha habari alama 02
iii/ Maneno yake mwenyewe alama 02
iv/ Idadi ya maneno alama 01
v/ Taratibu za uandishi alama 01

03 i/ Paa
- Paa limevunjika
- Mvuvi amepaa samaki

Alama 2 @ 1

ii/ Korongo
- Korongo limefurika
- Kaka amenunua korongo

Alama 2 @ 1

iii/ Uma
- Mama amenituma uma
- Tumbo lake linauma sana

Alama 2 @ 1

iv/ Paka
- Wana paka nyumbani kwao
- Baba anapaka ukuta wake rangi

Alama 2 @ 1

v) Uza
- Tunaki limeoza
- Ninemwoza binti yangu

Alama 2 @1

4. a) Juma alilima shamba vizuri

b) Sungura aliliwa

c) Bebe li jepesi mno

d) Shamba limelimwa vizuri

e) Mama amemkalisha mtoto

Alama 5 @1

5. Mwanafunzi achangamue sentensi kwa kuzingatia habari tano za uchangamuzi

Mwanafunzi wanachoza mpira mdogo, mwalimu anaandika barua ndefu.



Mwanafunzi wanachoza mpira mdogo, mwalimu anaandika barua ndefu

Alama 5 kila kutaja alama 1

6 a) Sentensi changamano
b) Sentensi Sahihi
c) Sentensi Sahihi
d) Sentensi Shurutia
e) Sentensi ambatano

Alama 5@1

7a i) Kiwakilishi
- Vizuri vyote vimeuzwa

ii) Kivumishi
- Viatu vizuri vimenunuliwa

iii) Kielezi
- Klarafunzi walicheza mpira vizuri

Alama 3@1

b i) Nomino
- Kizee amewasili asubuhi Sana

ii) Kivumishi
- Bibi kizee amejeruhiwa nyumbani

Alama 2@1

8. i) Shamirisho
Ni jina au kikundi jina kinachojaza nafasi ya mtendwa au mtendewa katika sentensi

ii) Chagizo
Ni neno au kikundi cha maneno kinachojaza nafasi ya kielezi katika tungo.

iii/ Upatanisho wa kisarufi

Ni hali ya viambishi vya maneno ndani ya tungo kukubaliana na kushikamana ili kuleta maana iliyokusudiwa.

Au

Inaangalia jinsi nomino inavyopatana na kiambishi awali cha kitenzi katika tungo

iv) Misimu

Ni maneno yasiyosanifu yanayozushwa na kikundi cha watu wachache na kushika kasi kwa muda mfupi kisha kutoweka, na yanayodumu husanifishwa na kuwa msamiati wa lugha husika.

v) Kamusi

Ni kitabu cha maneno yaliyopangwa kwa utaratibu wa alfabeti na kutolewa maana na maelezo mengine

Alama 10 @ 2

9. Mwanafunzi aandike barua ya kikazi kwa kuzingatia mambo yafuatayo:

i) Anwani ya mwandishi alama 01
ii/ Tarehe alama 01
iii/ Anwani ya mwandikiwa alama 01
iv/ Mwanzo wa barua alama 01
v/ Kichwa cha barua alama 01
vi) Utangulizi wa barua alama 01
viii) Kiini cha barua alama 04
ix) Mwisho wa barua alama 01
x) Saini, jina na cheo cha mwandishi alama 03
xi) Mpangilio wa kazi na taratibu za uandishi alama 01

10. Mwanafunzi atoe hoja zinazothibitisha ubantu wa kiswahili kwa kigezo cha kiisimu

UTANGULIZI

Isimu – Ni taaluma inayochunguza na kuchambua lugha kisayansi

KIINI

① Msamiati

kuna ufanano mkubwa wa msamiati wa lugha ya kiswahili na za kibantu

Mfano	Lugha	Nero
	kiswahili	Maji
	kizigua	manzi
	kinyakyusa	amisi

(ii) Tungo za kiswahili

Mfano

Lugha	kiima(K)	kitenzi (A)
kiswahili	Mama	anakunywa maji
kichaga	Nai	nainyo mringa
kihaya	Mae	manywa amaizi

iii) Upatanisho wa kisarufi

Mfano

Lugha

kiswahili Mama anakunywa maji

kigogo Yaya akunywa malenga

kisukuma Mayo alengwa minze

iv) Mnyambuliko wa vitenzi

Mfano	kiswahili	kucheka	kuchekesha	kuchekelea
	kigogo	kuseka	kusechesha	kusechelela

v) Mpangilio wa viambishi

Mfano

Kiswahili	a-na-kul-a
Kichaga	a-ke-ly-a
Kigogo	a-li-ly-a

Nafsi njeo Mzizi tamati maana

HITIMISHO

Mtahiniwa atoe maoni yake kuhusu ubantu wa kiswahili

ALAMA

Utangulizi	02
kiini hoja (5)	10@2
Hitimisho	03
Jumla	15

11. Mtahiniwa atoe maana ya riwaya, achague riwaya mbili kujibia swali kuthibitisha kuwa mwanamke ni nguzo ya jamii.

* Riwaya

Ni hadithi ndefu ya kubuni iliyonyumbuka kifani na kimaudhui na ambayo hutumia lugha ya masimulizi katika kuelezea visa na wahusika ambao huweza kuwa binadamu au wanyama kwa lengo la kusawirisha maisha ya jamii katika kipindi fulani

Hoja

Watoto wa Mama ntilie

- Mlezi wa familia - Mama ntilie na Jeni
- Mwajibikaji - Mama ntilie, kulwa, Zita
- Mwenye huruma - Jeni

Fakadini

- Mtu jasiri – Sekai, Shingai
- Mwenye mapenzi ya dhati – Sekai,
- Mwenye huruma – Shingai
- Mlezi wa familia – Sekai

Hitimisho

Mtahiniwa atoe msimamo wake kuhusiana na swali na ahusishe na jamii.

ALAMA

Utangulizi	02
Kiini hoja (\$)	12 @ 1½
Hitimisho	01
Jumla	15

12 Mtahiniwa aeleze maana ya dhamira

* Dhamira

Ni wazo au kusudio la mtunzi wa kazi ya fasihi

Hoja

Ngoswe Penzi kitovu cha uzembe

Jina linamaanisha kuwa mapenzi ni chanzo cha uovu katika jamii. Mtahiniwa ajadili dhamira zinazotokana na jina la kitabu kama

- Ukosefu wa elimu
- Ndoa za mitara
- Uchomaji wa takwimu
- Ndoa katika umri mdogo
- Umaskini

Orodha

Ni mlolongo wa vitu au majina ya vitu vilivyoandikwa. Mtahiniwa ajadili dhamira zi-

- Uaminifu
- Elimu
- Uwajibikaji
- Ukweli
- Upendo
- Uadilifu

Kilio chetu

Ni matatizo yanayoikabili jamii. Mtahini wa ajaribi matatizo yanayokabili jamii kama vile

- Ukosefu wa elimu ya kiinsia
- Athari za ukosefu wa hukumu kwa wenye UKIMWI
- Athari za mapenzi katika umri mdogo
- Athari za mila na desturi

Hitimisho

Mtahiniwa atoe mapendekezo juu ya mambo aliyoyajadili.

ALAMA

Utangulizi	02
Kiini hoja (8)	12 @ 1½
Hitimisho	01
Jumla	15